Mukhtasari Wa Mabishano Kwa Na Dhidi Ya Vikombe Vingi Vya Ushirika

(A Summary Of Arguments For And Against Individual Communion Cups)

Na

J D Logan

Mukhtasari Wa Mabishano Kwa Na Dhidi Ya Vikombe Vingi Vya Ushirika

(A Summary Of Arguments For And Against Individual Communion Cups)

Na

J D Logan

Mei 10, 2012

Mukhtasari Wa Mabishano Kwa Na Dhidi Ya Vikombe Vingi Vya Ushirika

(A Summary Of Arguments For And Against Individual Communion Cups)

(Ufuatao ni utangulizi unaotoka katika kitabu kidogo "Jenga Kulingana na Ramani". Iliyohaririwa 1925 katika "Ukristo wa Pacific" na ndugu wawili T C Hawloy na Eamost C Love, Ed.)

"*Watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana asema angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima.*" (Heb. 8:5).

"*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*" (2 Tim. 3:16-17). "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*" (Rum. 10:17).

Dini ya Yesu Kristo ni ufunuo kutoka kwa Mungu, na sio mageuko kutoka kwa mwanadamu. Ni mfumo wa wokovu kwa imani: hiyo ni, kwa kuamini kile ambacho Mungu amesema. Mamlaka ya ufunuo wa Mungu imetolewa na kumalizwa katika Biblia. Hakuna yeyote, kwa vile Yohana aliitimisha Ufunuo, amewezaa kunena kwa ajili ya Mungu kwa mamlaka, kama mitume walivyofanya; na kwamba Biblia ndio kiwango kamili na ramani kwa wanadamu wote kuendana nayo, kama wanapenda kufanya, kufanikiwa, safari ya kutoka duniani kwenda mbinguni.

Ambayo nitaongeza maneno ya Petro, "*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*" (2 Pet. 1:3).

Kwa vile mdahalo wa matumizi ya vikombe vingi umekuwa ukiendelea kwa zaidi ya miaka 100, mabishano mengi kwa na dhidi imependekezwa. Baadhi ya tarehe zifuatazo ni nyuma zaidi ya miaka 100 na zingine nimezisikia mwenyewe katika maisha yangu. Hakika ninataraji kwamba ukweli unaweza kutangazwa kwa kutoa neno la Yesu, kama Petro alivyosema, "*Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana, twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele.*" (Yoh. 6:68).

DHIDI YA WINGI

- Hazitambuliki kabisa katika Agano Jipya, hazijatamkwa hata na Kristo au mitume.
- Ni mapokeo yaliyoongezwa, tukiongea kimaandiko, zikiwa zimeanzishwa zaidi ya miaka mia iliyopita.
- Kanisa la Kristo iliziazima kutoka katika ulimwengu wa dini; chanzo kilekile ambacho jamii ya wamisionari walipotokea, vyombo vya mziki, ubatizo wa watoto wachanga, n.k. Tunapaswa kurudisha kila kitu ambacho tuliazima!
- Kuzitumia unakiuka barua ya sheria ya Kristo, maana kikombe kimoja pekee ndiyo inayoonyeshwa katika Agano Jipya.
- Kuzitumia unakiuka roho wa sheria ya Kristo kwa kufanya tendo la "kila mtu kuwa na kikombe chake" ambacho Kristo alikusudia kuwa "ushirika".
- Kuzitumia ni maafikiano ya maombi yetu ya umoja wa kimaandiko juu ya msemo maarufu usemao: "mahali ambapo maandiko hunena, tunanena; mahali ambapo maandiko yamenyamaza, tunanyamaza". Kiukweli hatuwezi kudai hivyo, wakati tunatumia vikombe vingi.
- Kuzitumia ukiuka mfano wa Kristo katika kuanzisha huduma ya ushirika. "*…alitwaa kikombe*
- Kuzitumia unakiuka agizo la wazi la Kristo, aliyesema: "*Nyweni nyote katika hiki*".
- Kuzitumia unavuja amani na ushirika mzuri kati ya makusanyiko, kwa wale wanaopinga vikombe hawawezi kuabudu nao, hata kidogo kuliko wanavyofanya na vyombo vya mziki.
- Kuzitumia unakiuka ujumbe wa mwisho kutoka mbinguni unaokataza "kuongeza katika" sheria ya Mungu au maagano.
- Kuzitumia unafanya ibada ya "bure" kwa maana inaondoa maandiko ya Agano Jipya, "*…maagizo ya wanadamu.*" (Marko 7:7).
- Kuzitumia kunaangamiza ishara ile ya amani kama ilivyo elezwa katika 1 Kor.10:16-17, ikisisitiza umoja wa "*… mwili*" na damu.

- Kuzitumia kunapaswa kusitishwa mara moja, maana Kristo alisema, "*Kila pando asilolipanda Baba yangu aliye mbinguni, litang'olewa*". (Mat. 15:13).

KWA UPANDE WA WINGI

- Siyo "vizuri" kunywa baada ya mwingine. Hatufanyi hivyo katika miji zetu.

  Jibu…katika familia ambapo kuna upendo wowote wa kweli mtu anaweza kunywa baada ya mwingine na asifikirie chochote. Mara nyingi hufanyika. Hakuna kinacho patikana kwa kuwa "mwema". Baadhi ya watu ni "wema" sana kwa ulimwengu huu.

- Ndugu fulani na fulani ni wachafu; anavuta tumbaku na kuingiza ndevu zake katika kikombe; na mara nyingi hasafishi pua lake, n.k.

  Jibu…Hili halina ubishi wa vikombe vingi. Mtu anapaswa kumwambia ndugu fulani na fulani kujisafisha. Kijana wa Samweli alipotenda dhambi, watu waliomba wapewe mfalme. Walichotakiwa kufanya ni kuwasafisha waamzi. Walilivunja taifa kwa kubadilisha agano la Mungu badaala ya kuwarekebisha wale waliokuwa na hatia. Ebu tuziepuke makosa yao.

- Sheria ya Amerika inakataza kikombe kimoja.

  Jibu…Ndiyo kuna sheria katika baadhi ya sehemu ambazo ni kinyume na "kikombe kimoja", lakini hakujawahi kuwa na juhudi katika kuzifanyia kazi kwenye mambo ya dini na labda haitakuwepo. Lakini kunapaswa kuwepo na juhudi zinazoleta mkanganyiko katika ibada, ebu Kristo asimame aliposimama Petro na kusema, "*Tunapaswa kumtii Mungu kuliko mwanadamu*", na kwa ukali tuchukue matokeo.

- Kuna hatari ya kukumbana na magonjwa ya hatari katika kikombe kimoja.

  Jibu…Ndiyo, madaktari na wanasayansi watatuambia hivyo. Hataivyo, wanafunzi wameonyesha kwamba kuna hatari kubwa kwenye mikono michafu kwamba kutoka katika kikombe kimoja. Ikiwa kikombe kimoja ni kitu hatari, basi kanisa la Kristo lingekufa zamani sana. Kwa miaka mia hadi kurudi katika karne ya ishirini, waumini wa huu mwili mkuu katika taifa hili kubwa wamekutana na kushiriki katika kikombe cha ushirika. Wana afya na wenye nguvu kama mwili wowote wa kidini ninao ufahamu. Ikiwa sehemu ya hadithi ni kweli, kama wengine wanvyotaka tuamini, kwa kujali kupata magonjwa katika kukinywea kikombe cha ushirika, sote tungekuwa tumeshakufa kabla ya wanabaiolojia" kugundua tatizo. Tumueshimu Mungu kuliko vijidudu!

Kinyume na hilo, kama kuna mgonjwa wa kifua kikuu katika kusanyiko, kusanyiko lote litakuwa limekumbwa na tatizo la upumuaji. Vijidudu hivi haviambukizwi kwa kukinywea kikombe.
Pia, vikombe tofauti vinapoanzishwa, mwenye ugonjwa bado anashikilia mkate na anauhakika kuacha vijidudu kwenye mkate, afuataye atapata wadudu. Piua vikombe hivi vinapotumika mara moja, huoshwa na kutunzwa hadi ibada ijayo. Isipokuwa zinachemshiwa maji kila wakati, wadudu ambao wako kwenye vikombe hivyo haziwezi kuuawa, bali zinasambazwa katika vikombe vingine
Pia, kumbuka, wadudu wa kifua kikuu inasemekana wanabaki hai na ni hatari kwa miezi sita chini ya hali nzuri. Kinachomzuia mtu kupata mmoja wa wadudu hao walio hai juma pili ijayo ni nini?
Hitimisho …Kuna hatari kidogo katika kukinywea kikombe cha ushirika, kama ipo, na vikombe vingi hawaondoi Atari yote inaweza kuwepo.

- Wahubiri wetu viongozi uzihidhinisha.

  Jibu …Hivyo ndivyo inavyoweza kusemwa kuhusu Jamii ya Wamisionari, vyombo vya mziki, mkate wa kumega kila mtu kuchukua wake, na kila aina ya utungwaji ambao umeenea katika amani ya ndugu na kuharibu njia ya kwenda mbinguni. Baadhi ya watu wamekwenda visivyo, hivyo ndivyo!

- Makanisa yetu yote yameongoza kwa kuzianzisha.

  Jibu …Hii inafanana na Nambari 5. Yalikuwa ni makusanyiko “yaliyostaarabika” katika miji mikubwa ambao walianza kuzitumia. Hii ilifanyika mara zote kwa kushindana na madhehebu. Ilichukua miaka kadhaa ya mpito kwa hili kuweza hitimishwa. Mengi ya makanisa haya leo zimeanzisha kila aina ya matendo yasiyo ya kimaandiko. Nimesoma kuhusu vijana wakienda na gitaa katika madarasa ya biblia. Baadhi ya makusanyiko “endelevu” wanawatumia wanawake kusimamia ushirika wa meza ya Bwana. Ukianza kutoka katika ramani ya kimaandiko, hakuna njia nyingine yoyote unayoweza ili ushinde upotovu kikamilifu!

- Tunatumia vikombe viwili (wakati mwingine vitatu), kwa nini visiwe mia mbili?

  Jibu …Hakika ni sawa! Kwa nini visiwe mia mbili? Hakuna kusanyiko linalotumia vikombe viwili, au zaidi kwa mamlaka ya Kristo. Aliye anzisha tendo hili, sifahamu. Lakini kitu kimoja kwa hakika, ni kwamba tendo hili halikuanzishwa na Kristo wala mitume. Hii haiwezi kutumika kama ubishi kwa ajili ya vikombe vingi, hadi mamlaka ya wawili zithibitike.

- Neno “kikombe” ni mfano.

Jibu …Wakati mwingine hii ni kweli, lakini siyo kila mara. Yesu alipo "*twaa kikombe*", alichukua kikombe halisi; katika hili hakuwezi kuwa na shaka. Hataivyo, hii haitowi mamlka kutumia vikombe vingi. "*Maana kila muulapo mkate huu, na kukinywea kikombe, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*" (1 Kor. 11:26). Tuchukulie kwamba huu ni mfano, mbadala, alafu nini? Katika shauri hili chombo kinawekwa kwa kitu kilichobebwa. Chombo ni nini? "*kikombe*". Ni nini kilichobebwa? "*uzao wa mzabibu*".
Kristo aliomba, "*Baba ikiwa ni mapenzi yako kikombe hiki kiniepuke.*" (Luka 22:42). Hapa tunaambiwa kwamba kikombe ni mfano, hakukuwa na kikombe halisi. Hiyo ni kweli. Yesu alikuwa anaongelea mfumo wa mateso uliokuwepo kwa wakati ule; ule wa kumlazimisha mteswaji kukinywea kikombe kilicho na uchafu, sumu inayouwa. Hii haisaidi katika matumizi ya vikombe vingi.

- Ni kilichomo ndani ya kikombe ndio kinahesabiwa, chombo hakihesabiwi.

  Jibu…Wayahudi walikuwa na ubishi unaofanana na huu. "Naye aapaye kwa hekalu, huapa kwa hilo, na kwa yeye akaye ndani yake." (Mat. 23:16 – 22).
  Kwa mukhutasari jibu la Yesu tunalo: "Vipofu ninyi maana ni ipi iliyo kubwa, faharisi, au kikombe kinachotakasa faharisi?"

- Yesu alisema, "Nyweni nyote katika hiki (kikombe)."

  Jibu …Hii haitowi faraja kwa wale wanaotumia vikombe vingi, maana hii haikuwa "*kikombe cha Bwana*", bali kikombe cha Pasaka. Hataivyo, kwa "*kikombe cha Bwana*", tunafahamu jinsi walivyo kinywea wenyewe: "*…wote walikinywea.*" (Marko 14:23).

- Hakuna awezaye kukinywea kikombe halisi…hiyo ni, hakuna awezaye kumeza sehemu ya kikombe halisi.

  Jibu… "*Tuna madhabahu ambao wale waihudumiao ile hema hawana ruhusa kula vitu vyake.*" (Heb. 13:10). Hapa, wengine husemwa kula vitu vya hema. Kama mtu atakula vya madhabahu kwa kula vitu vilivyotolewa katika hema, mtu anaweza kukinywea kikombe kwa kunywa kilichomo ndani yake. "*…Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani.*" (1 Kor. 10:21). Hapa wengine husemwa kuwa wanakula meza. Kila mtu anafahamu kwamba katika kula kilichopo mezani, hitaji kamili ya lugha hii imetimizwa.

- Tuna ushirika wetu na Mungu, hataivyo, haileti tofauti ni vikombe vingapi tunavyotumia.

  Jibu …Ubishi huu unafanya kusanyiko limege mkate wote pasipo sababu. Kama washiriki wengine katika kusanyiko hawatazami katika ushirika wa meza ya Bwana, kwa nini tunakutana? Mtu anaweza kuwa na ushirika na Mungu nyumbani au nje porini. Makosa haya yanasababishwa na kutokuelewa neno "ushirika".

Kuhusu neno hili, kamusi ya Vine inasema, “koinonia’, kuweka katika desturi (koinos), ushirikiano, ushirika, manisha…kushiriki katika ukumbusho ya dhamana ya damu (kifo) cha Kristo na mwili wa Kristo, kama ilivyo kielelezo katika Meza ya Bwana, 1 Kor. 16:16,” (Vine uk 115). Huwezi kuwa na ushirika wewe mwenyewe!

- Swali la “kikombe” ni swali lisilofundishika.

  Jibu…Kwa heshima tunaeleza kwamba kikombe kimeonyeshwa hasa kila wakati chombo kinapo tajwa. Yesu alitwaa kikombe alipokuwa anaanzisha. Baadae, Paulo alipokuwa anatoa kwa kanisa alichokuwa nacho “*pokea kutoka kwa Bwana*”, anaainisha kikombe. Hii imefundishwa. “*kikombe cha Bwana*” imewekwa wazi zaidi katika maandiko kuliko siku ambayo ingenywewa. Alafu ubishi juu ya “*siku ya kwanza ya juma*” kama siku ya kukusanyika Wakristo inatosha sana. Ama ni swali ambalo halijafundishwa!

- Kusema kanisa linapaswa kuwa na kikombe kimoja ni “kuweka sheria sehemu ambapo Mungu hakuweka”.

  Jibu …Hii ingeweza kuwa kweli kama Bwana mwenyewe asingeanzisha, kwa kutumia kikombe kimoja, na kuagiza, “*Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu*”. (Luka 22:19). Je tunamwekea Mungu sheria tunapowaimiza watu wote wanaokuja kanisani kwenda katika maji ya ubatizo na kuzikwa pamoja na Bwana katika ubatizo? Hapana! Kwa nini? Kwa sababu Biblia inafundisha hivyo yenyewe. Sheria iliwekwa na Kristo, mwenyewe! Kwa kusisitiza hilo ndugu wanapaswa kutumia nyingi, na sio vikombe zaidi kuliko vinavyoonyeshwa katika maandiko, mtu haweki sheria kwa Mungu.

- Kanisa la Yerusalemu lilikuwa kubwa kiasi kwamba wote wasingeweza kukinywea kikombe kimoja.

  Jibu…Huu ni ubishi ule ule unaofanywa na wanaochanganya kwamba kunyunyiza au kumwaga ni sahihi, kwa sababu watu elfu tatu wasingeweza kuzamishwa kwa siku moja. Lakini tunajibu kwa kuonyesha kuwa hakukuwa na sababu kwa mtu mmoja kuwabatiza wote. Hakuna sababu ya kuamini kuwa ndugu wote Yerusalemu walijaribu kumega mkate katika mkutano mmoja.
  Pia, tunaweza kuuliza, Ikiwa, unavyopendekeza, wote katika kanisa la Yerusalemu walikutana katika mkutano mmoja, je walitumia vikombe vingi na zaidi ya vyombo elfu tatu? Tunapaswa kukumbuka kuwa hivi havikuwepo hadi karibia miaka elfu mbili baadae!
  Hakuna mkate unaoweza kutengenezwa unaoweza kuwatosha zaidi ya watu elfu tatu, alafu Paulo anasema, “*sote ni washirika katika mkate huo mmoja.*” (1 Kor. 10:17). Hakika kuna mamlaka zaidi hapa kwa wingi wa mikate kama ilivyo kwa vikombe. Na kama kusanyiko linaweza kupata mamlaka ya vikombe vingi katika maandiko, hakika, kwa hali hiyo, inaweza pia kupata

mamlaka ya kuwa na mikate mingi (wefa). Sasa kwa nini tunawapinga Roman Katholiki katika shauri hili, kama tunavyofanya?

Ilikuw ni desturi ya Wayahudi kushiriki Pasaka kila wakati. Familia na mwanakondoo ndio walikuwa sehemu ya ibada. Lakini familia na mwanakondoo mara zote hawawi hivyo, kama matokeo, wakati mwingine familia walipaswa kujirudia. (angali Kutoka 12:4). Lakini sheria ilikuwa ni "*…mwanakondoo wa nyumba.*" (ms3). Hakuna Myahudi ambaye angefikiri kusema, "Familia yangu ni kubwa sana, nitachinja wanakondoo wawili." Mwanakondoo mmoja; mji mmoja.

Kwa Wakristo kusanyiko na kikombe ni umoja wa ibada, Kama kunaweza kuwa na mabadiliko kwa sababu ya idadi, inaweza kuwa hiyo ya kusanyiko, siyo idadi ya vikombe. Nimewahi kuwa katika kusanyiko lililo na waumini kati ya mia hamsini na mia mbili na walikuwa wanahudumiwa kirahisi kwa kikombe kikubwa (kikombe). Kama kusanyiko linakuwa kubwa, tunapaswa kuruhusu kusanyiko lingine lianzishwe, na hivyo kutangaza kazi katika sehemu zingine.

· Kupinga vikombe vingi inasababisha mgawanyiko.

Jibu…Hili haliwezi kukataliwa, kama matumizi yake yanaendelea, au kama baadhi ya watu wanasisitiza katika kuanzisha vyombo vya mziki. Leo, tunawaheshimu ndugu waaminifu waliozeeka sasa waliokuwa kinyume na mkanganyiko huu na kama matokeo, waliliokoa kanisa. Leo hii, tunaendelea kukumbwa na adha ileile juu ya matumizi ya vikombe vingi. Lakini kuna sababu moja iliyobaki kwa wana wa Mungu; shikilia mfumo wa kweli wa ibada ya Mwokozi kwa gharama yoyote. Kama mgawanyiko lazima iwepo, na tayari ipo, na itakuwa, wengi watapotea kwa sababu ya ukengeufu, lakini watakaobaki wataokolewa. Lakini wote wakijikabidhi katika upotovu, Bwana atakuja na kukiondoa kiambaza chao katika sehemu yake na watapotea. Hataivyo, Bwana, hatalaumu mgawanyiko juu ya wale watakao baki waaminifu katika neno lake na ahadi. Hatuitaji kuwa na uoga juu ya hili.

(Kuna ubishi mwingine mwingi unaotumiwa kutetea matumizi ya vikombe vingi, lakini hii zaidi au kidogo inawawakilisha wale wa miaka mia iliyopita. Tunawasihi ndugu zetu wanaoshiriki katika huu upotovu kutoka katika kweli kuacha hili na warudi katika ibada ya kweli kulingana na maandiko.)

J D Logan